# Matembezi ya siku moja ya kulala ya safari za kishule

Kuna mengi ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza shuleni linapokuja suala la maarifa ya kitaaluma na ujuzi wa kijamii. Wakati mwingine mahali pazuri pa kujifunza ni nje ya darasa.





Kwa mfano, inaweza kuwa muhimu kutembelea jumba la makumbusho linaloonyesha maonyesho kuhusu mada au mafundisho ambayo darasa linashughulikia. Ikiwa mada ni samaki na maisha ya baharini, inaweza kuwa vizuri kutumia siku ya shule kando ya bahari na vifaa vya uvuvi. Wanafunzi wanapojifunza kuhusu msitu, ni wazo zuri kutumia siku msituni. Kile ambacho wanafunzi wanajifunza katika matembezi haya kinatoa msingi mzuri kwa kazi zaidi za shule.





Mafunzo nje ya darasa yanaweza kutoa fursa bora za kujifunza ujuzi wa vitendo kwa kushirikiana na wanafunzi wenzao. Katika matembezi, wanafunzi wanapata nafasi ya kuchunguza mazingira wanayoyajua na wasiyoyajua. Wanakabiliwa na changamoto katika mazingira salama na wanaweza kuonyesha pande mbalimbali za wao wenyewe. Mbali na mafunzo yote yanayotokea katika matembezi mbalimbali, ni fursa nzuri ya kufahamiana kwa njia tofauti na zile za shuleni.

Brosjyren er laget av Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring i samarbeid med Utdanningsdirektoratet. Illustrasjonene er laget av Redant

# Kambi ya shule (kambi ya kulala ya kimasomo)

Wanafunzi wote katika shule za Norway wanapewa nafasi ya kwenda kwenye kambi ya shule wakati fulani katika kipindi cha elimu yao ya lazima. Wanafunzi huenda pamoja na walimu wanaowajua kwenye kambi ya shule ili kujifunza ujuzi mpya. Kambi hizi pia zina walimu wao wenyewe ambao wanajua sana kuhusu eneo linalozunguka kambi na kuhusu shughuli ambazo wanafunzi watashiriki. Shughuli katika kambi ya shule ni za afya, za kusisimua na za kielimu. Mengi ya maarifa na ujuzi waliyojifunza katika kambi ya shule yatakuwa ya manufaa na ya kukumbukwa kwa maisha yote.





Wakati madarasa yanakwenda kwenye kambi ya shule au kwenye safari nyingine za kulala, wakati wa usiku, wavulana hulala katika bweni moja na wasichana katika bweni lingine. Walimu wanawajibika kuhakikisha kuwa vyumba ni tulivu na vya mpangilio. Hii huunda mazingira salama na uzoefu mzuri kwa wanafunzi. Kila mtu anapaswa kujisikia salama katika safari za darasa.





Wanafunzi wengi wanaweza kuwa na mahitaji maalum ya lishe. Shule itajitahidi kutosheleza mahitaji haya. Pia ni jukumu la shule kuhakikisha usalama wa wanafunzi.

Matembezi yanayoandaliwa na shule ni bure. Shule nyingi na kambi za kimasomo za kishule pia zina vifaa ambavyo wanafunzi wanaweza kukopa.

Tafadhali zungumza au ongea na mwalimu ikiwa una maswali yoyote kuhusu matembezi au kambi ya shule, au ikiwa mtoto wako ana mahitaji maalum ambayo shule inapaswa kujua.

Brosjyren er laget av Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring i samarbeid med Utdanningsdirektoratet. Illustrasjonene er laget av Redant